SHULE YA SEKONDARI SALE,

S.L.P.76,

LOLIONDO.

03/12/2018.

Kumb. Na……..
Jina la mwanafunzi ……..
Shule atokayo……

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SALE WILAYA YA NGORONGORO, MKOA WA ARUSHA, MWAKA 2019.</u>

1.0. Utangulizi

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2019. Shule ya sekondari Sale iko umbali wa kilometa 50 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Kuna usafiri wa kutoka Loliondo hadi shuleni kila siku kwa basi, nauli ni **Tsh.7,000/=.** Shule itafunguliwa **tarehe 04/01/2019** siku ya jumatatu, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia saa 2 asubuhi hadi saa 10:00 jioni. Ukichelewa kuripoti shuleni nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwenye ari ya kusoma aliyekosa chaguo la kwanza. Mwisho wa usajili wa kidato cha kwanza ni **tarehe 21/01/2019** siku ya jumatatu.

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1. Sare ya Shule

a. Sare ya shule hii ni suruali za **Dark Blue** (2) kwa Wavulana na Wasichana sketi (2) za rangi ya **Dark Blue**, tumia sample ya kitambaa tulichokubandikia, Suruali iwe na marinda mawili (2) na mikunjo kwa chini (Turn up) mashati meupe mawili kwa wavulana na wasichana yenye mikono mifupi.
   - Viatu pea (2) vyeusi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba (vyenye kamba)
   - Soksi nyeusi kwa Wavulana na nyeupe ndefu kwa wasichana pea -4.
   - Tai ya **Dark Blue**
   - Sweta la rangi ya **Dark Blue**
   - T-Shirt ya blue yenye nembo ya shule pea mbili kwa wanafunzi wote. Nembo imeambatanishwa.

b. Sare ya kushindia au shambadress.
   - Wavulana **Damu ya Mzee** pea mbili (2)
   - Wasichana **Damu ya Mzee** pea mbili (2)

c. Sare za michezo kwa shule hii.
   - Tracksut ya blue yenye mistari mweupe pembeni
   - Raba rangi yoyote ya michezo.
     NB: Mzazi hakikisha kuwa nguo zote zinawekwa alama kwa cherehani.

3.0. Vifaa vya masomo

- ✓ Uje na counter book 9 (quire 2 or 3), daftari za graph (Graph pad) 1, madaftari madogo **kumi (10)** na kalamu za kutosha.
- ✓ Mathematical set

- ✓ Dictionary (Oxford) English to English.
- ✓ Begi la kubebea madaftari na vitabu (mifuko ya plastiki ni marufuku)
- ✓ Mnunulie mwanao saa ya mkononi ili aweze kutunza muda.
- ✓ Unaombwa umnunulie mwanao vitabu vya kutosha.
    i. Biology Book one (Oxford)
    ii. Physics Book one (Oxford)
    iii. Mathematics Book One(oxford)
    iv. Kiswahili kidato cha kwanza (oxford)
    v. English book one (oxford)
    vi. Civics book one (oxford)
    vii. Geography book one (oxford)
    viii. History book one (oxford)
- ✓ Faili moja kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake.(spring file)

4.0. vifaa vingine

- ✓ Aje na godoro Nchi (3) lenye upana wa futi mbili na nusu kwa 6.
- ✓ Sanduku la bati kwa ajili ya kutunza vifaa vyake.
- ✓ Aje na ufungio wa chelewa.
- ✓ Aje na ndoo ndogo ya kuogea.
- ✓ Aje na taulo na kanga mbili kwa wasichana
- ✓ Msichana aje na pedi packet 4
- ✓ Aje na sahani, kikombe, bakuli na kijiko visiwe vya Plastiki
- ✓ Aje na sabuni za kutosha, dawa ya meno, mswaki na mafuta ya kupaka yasiyo na harufu kali.
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vyakula.
- ✓ Mpatie mwanao fedha za matumizi (pocket money) angalau 20,000/=au Zaidi.
- ✓ Aje na toilet paper pactet 5 au 6
- ✓ Shuka mbili (2), rangi ya pinki kwa wavulana na blue kwa wasichana.

5.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya RAIS - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, Wazazi, wafanyakazi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa wanafunzi wanapokuwa katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i. Kutunza mali za umma.

5.1. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

a. Wizi
b. Uasherati na ushoga
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e. Kupigana na kupiga
f. Kuharibu kwa makusudi mali za Umma
g. Kudharau Bendera ya Taifa
h. Kuwa mjamzito / kupata mimba
i. Kuoa au kuolewa
j. Kutoa mimba
k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l. Kukataa adhabu kwa makusudi
m. Kuwa na simu ya mkononi.

MUHIMU.

a. Anatakiwa apimwe kuthibitisha afya yake kwenye hospitali ya Serikali. Fomu imeambatanishwa kwenye barua hii.
b. Shule haitoi chakula maalum kwa wagonjwa (special diet)
c. Simu haziruhusiwi hapa shuleni (Ukikamatwa na simu utarudishwa nyumbani)
d. Tafadhali soma kwa makini maelekezo /maagizo hayo na kuyatekeleza kwa umakini.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SALE

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA 0627398260/0786725044 (MKUU WA SHULE) AU 0626667161 (MAKAMU MKUU WA SHULE).

……..

NGUNAI G. GIDORE.

MKUU WA SHULE.

NAKALA:

1. Mkaguzi Mkuu wa Shule,
   Kanda ya Kaskazini Magharibi,
   S.L.P 807,
   ARUSHA.

2. Afisa Elimu (M)) Arusha,
   S.L.P 3032
   ARUSHA.

3. Mkurugenzi mtendaji,
   Halmashauri ya (W) Ngorongoro,
   S.L.P 01.
   LOLIONDO.